# CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

**NDAKI YA MISITU, WANYAMAPORI, NA UTALII**

**IDARA YA TATHIMINI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MISITU**

**MUHTASARI WA TASNIFU**

**JINA LA UTAFITI: ATHARI ZA MPANGO WA UTHIBITISHAJI WA KIKUNDI WA FSC KATIKA HALI YA MISITU NA MAISHA YA JAMII NDANI YA HIFADHI ZA MISITU YA ARDHI YA VIJIJI, WILAYA YA KILWA, TANZANIA.**

**JINA LA MWANAFUNZI: NSAJIGWA NASSAN KATUNGILA**

**WASIMAMIZI: PROF. GIMBAGE E. MBEYALE,**

**DR. KAJENJE M. NKUKURAH**

**MEI, 2026**

## 1.0 UTANGULIZI

Usimamizi wa Misitu Shirikishi unaotekelezwa na Jamii (Community Based Forest Management – CBFM) umeonekana kuwa nyenzo muhimu katika kuhamasisha usimamizi endelevu wa misitu pamoja na kuboresha maisha ya jamii zinazotegemea rasilimali za misitu. Tathmini ya athari za uthibitishaji wa misitu katika hali ya misitu na maisha ya jamii ndani ya Hifadhi za Misitu ya Vijiji (VLFRs) chini ya mpango wa uthibitishaji wa kikundi wa FSC ilifanyika kusini mwa Tanzania kwa kuangazia Hifadhi za Misitu za Long'ou na Mbumbila B zilizopo katika vijiji vya Likawage na Nanjirinji A mtawalia. Mpango huu ulianzishwa ili kuonesha namna usimamizi bora wa misitu unavyoweza kuboresha hali ya misitu na maisha ya wananchi kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za misitu.

Ingawa tafiti nyingi zimefanyika kutathmini utendaji wa mifumo mbalimbali ya usimamizi wa misitu nchini Tanzania, ni tafiti chache zilizojikita katika kutathmini mipango ya uthibitishaji wa misitu. Aidha, bado kuna uelewa mdogo kuhusu kiwango ambacho mpango wa uthibitishaji wa kikundi wa FSC umefanikiwa kufikia malengo yake ya msingi ya kuboresha maisha ya jamii na hali ya misitu katika VLFRs. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kubaini muundo wa jamii za miti, uoto mpya (regeneration), na muundo wa misitu kabla na baada ya uthibitishaji wa FSC, pamoja na kutathmini mchango wa uthibitishaji huo katika hali ya maisha ya jamii zinazoshiriki kusimamia hifadhi za misitu chini ya mfumo wa VLFRs kama mojawapo ya aina za CBFM.

Utafiti ulitumia mbinu mseto (Mixed Methods Approach), ambapo ukusanyaji wa takwimu za kibaolojia ulifanyika kwa kutumia *systematic sampling* ili kupata taarifa za muundo wa misitu na uoto mpya. Kwa upande wa taarifa za kijamii na kiuchumi, mbinu zilizotumika ni pamoja na dodoso kwa kaya, majadiliano ya vikundi lengwa (FGD), mahojiano na watoa taarifa muhimu pamoja na uchunguzi wa moja kwa moja msituni.

Takwimu zilichambuliwa kwa kutumia programu za SPSS toleo la 24.0 na Excel. Takwimu za kibaolojia zilichambuliwa kwa kutumia kanuni na kukokotoa viashiria vya utawala wa miti, huku miti iliyopo na usambazaji wake ukikokotolewa kwa kutumia Kielezo cha Shannon-Wiener. Msongamano wa miti na ujazo wa miti vilikokotolewa kwa kutumia kanuni. Takwimu za kijamii na kiuchumi ziliorodheshwa, kujibiwa kwa kuweka misimbo na kuchambuliwa kwa kuandaa jedwali na matriksi zilizolinganisha majibu kwa kila kijiji. Matokeo yaliwasilishwa kwa kutumia majedwali, grafu na chati kupitia takwimu elezi kama wastani, mediani, asilimia na idadi.

## 2.0 MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti ulibaini kuwa Mpango wa Uthibitishaji wa Kikundi wa Forest Stewardship Council (FSC) una mchango mkubwa katika kuboresha hali ya misitu ndani ya Hifadhi za Misitu ya Vijiji katika Wilaya ya Kilwa, Tanzania. Misitu iliyothibitishwa ilionyesha uboreshaji wa muundo wa misitu, kuongezeka kwa msongamano wa miti, eneo msingi kubwa zaidi pamoja na uoto mpya wenye afya ikilinganishwa na hali ilivyokuwa kabla ya uthibitishaji. Hali ya uoto mpya ilionesha uwepo mzuri wa miti michanga, huku mgawanyo wa kipenyo cha miti wenye umbo la "Inverse J-shaped" ukionesha uwepo wa mfumo imara na endelevu wa ikolojia ya misitu. Aidha, ongezeko la jamii za miti, viashiria vya ndege lilionesha kuwa uthibitishaji umechangia katika uhifadhi wa bioanuwai na kuboresha ubora wa makazi ndani ya hifadhi za misitu.

Vilevile, utafiti ulionesha kuwa uthibitishaji wa FSC umechangia kuboresha maisha ya jamii zinazoshiriki kusimamia misitu iliyothibitishwa. Jamii zilinufaika kupitia kuongezeka kwa fursa za ajira, upatikanaji wa masoko ya kimataifa kwa bidhaa za misitu zilizothibitishwa, kuimarika kwa ushiriki wa wananchi katika usimamizi wa misitu pamoja na kuongezeka kwa uwezo wa jamii katika matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Hata hivyo, utafiti pia ulibaini changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa uthibitishaji huo, ikiwemo uhaba wa rasilimali fedha, upungufu wa utaalamu wa kiufundi na changamoto za miundombinu. Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kuwa uthibitishaji wa kikundi wa FSC ni nyenzo muhimu katika kuhamasisha usimamizi endelevu wa misitu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi chini ya mfumo wa Usimamizi wa Misitu Shirikishi nchini Tanzania.

## 3.0 UMUHIMU WA UTAFITI

Utafiti huu unatoa ushahidi muhimu kuhusu namna uthibitishaji wa kikundi wa FSC unavyochangia usimamizi endelevu wa misitu, uhifadhi wa bioanuwai na uboreshaji wa maisha ya jamii ndani ya Hifadhi za Misitu ya Vijiji nchini Tanzania. Matokeo ya utafiti yanaweza kusaidia watunga sera, wasimamizi wa misitu, mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na jamii za maeneo husika kuelewa faida za kiikolojia na kijamii zinazotokana na uthibitishaji wa misitu, ikiwemo kuboreka kwa hali ya misitu, kuongezeka kwa uoto mpya wa miti, fursa za ajira na upatikanaji wa masoko ya bidhaa za misitu zilizothibitishwa. Aidha, utafiti huu unaziba pengo la maarifa kuhusu mipango ya uthibitishaji katika misitu inayosimamiwa na jamii, na kutoa taarifa muhimu kwa tafiti zijazo, utungaji wa sera na upanuzi wa matumizi ya usimamizi endelevu wa misitu nchini Tanzania na kwingineko.

## 4.0 MAPENDEKEZO

i. Kuimarisha upatikanaji wa masoko na uhusiano wa biashara kwa bidhaa za misitu zilizothibitishwa ili kuongeza manufaa ya kiuchumi kwa jamii zinazosimamia Hifadhi za Misitu ya Vijiji.
ii. Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na wadau wengine wanapaswa kutoa msaada wa kifedha na kiufundi, kuboresha miundombinu, kurahisisha taratibu za uthibitishaji na kuweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa uthibitishaji wa kikundi wa FSC.
iii. Kufanyika kwa tafiti zaidi zinazolinganishwa kati ya misitu iliyothibitishwa na isiyothibitishwa ili kuelewa kwa kina athari za muda mrefu za kiikolojia na kijamii zinazotokana na uthibitishaji wa misitu.